

Maswali

1. Yesu alikuwa amewaahidi Wanafunzi nini?
2. Wayahudi wengi kutoka nchi mbali mbali walikuwa wamekuja nini Yerusalemu?
3. Nini ilifanyika wakati wanafunzi walikuwa pamoja wakisali?
4. Wanafunzi walifanya nini walipojazwa kwa Roho Mtakatifu?
5. Mbona Wayahudi walishangaa?
6. Watu wachache walidhihaki wakisema nini?
7. Petro alisema nini juu ya kuzungumza kwa lugha tofauti?
8. Petro aliwambia Wayahudi walifanya nini chenye kilikuwa kiovu sana?
9. Petro aliwambia Wayahudi wafanye nini?
10. Watu wangapi walibatizwa siku hiyo?

Majibu

1. Yesu aliahidi wanafunzi kuwapa nguvu za Roho Mtakatifu.
2. Wayahudi walikuwa wamekuja kutimiza siku kuu ya Pentekoste.
3. Kelele kama upepo wa nguvu. Ndimi kama myiale za moto zilitua juu ya wanafunzi. Walijazwa na Roho Mtakatifu.
4. Wanafunzi waliweza kuzungumza kwa lugha tofauti tofauti.
5. Wayahudi kutoka kwa nchi mbali mbali walielewa lugha zilizozungumzwa.
6. Kulikuwa na watu wachache waliowafanyia wanafunzi msaha wakisema kwamba walikuwa wamelewa.
7. Wanafunzi walizungumza lugha tofauti kwa nguvu za Roho Mtakatifu.
8. Petro aliambia Wayahudi kwamba walikuwa wamemsulibisha Yesu, ndiye Mwana wa Mungu.
9. Petro aliambia Wayahudi wajute sana na watubu.
10. Watu kama elfu tatu walibatizwa siku hiyo.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 2 Mwaka wa 2

88 Siku ya Pentekoste

Kwa Biblia

Matendo ya Mitume mlango wa 2; Yoeli mlango wa 2: 28 – 32


Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu alipea wanafunzi nguvu ili iwasaidia kuhubiri Injili kwa mataifa yote


Somo

Wanafunzi waliona Yesu alipokuwa akienda kuishi mbinguni na Mungu. Walienda kukaa Yerusalemu. Yesu alikuwa amewaahidi nguvu za Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu angesaidia wanafunzi kuhubiri Injili kwa mataifa yote. Wanafunzi waliingojea wakiwa Yerusalemu.

Ilikuwa siku kuu ya Pentekoste. Wayahudi wengi kutoka kwa mataifa mbali mbali walikuja Yerusalemu kutimiza siku kuu hiyo. Wanafunzi walikaa pamoja. Walikuwa wakiomba Mungu. Bunde si bunde walisikia sauti kama ya upepo ukivuma na nguvu. Huo upepo uliendelea kuongeza sauti na ukajaza nyumba. Wanafunzi waliona ndimi kama mwali wa moto. Hizo ndimi zilitua juu ya kila mwanafunzi. Wote wakajazwa na Roho Mtakatifu. Walianza kuzungumza kwa lugha tofauti zenye hawakuwa wamejifunza.



Siku hiyo Wayahudi wengi walikuwa wamekuja Yerusalemu. Walikuwa wamekuja kutimiza siku kuu ya Pentekoste. Hawa Wayahudi walizungumza lugha nyingi tofauti tofauti.



Wayahudi walisafiri mpaka Yerusalemu kuadimisha Siku kuu ya Pentekoste. Wanafunzi waliweza kuzungumza na hao watu kwa lugha zao.

Umati wa watu ulikusanyika kuangalia ni nini ilikuwa imesababisha hizo kelele. Wanafunzi walikuwa wanazungumza kwa lugha nyingi tofauti tofauti. Waliweza kuzungumza kama lugha 17 zilizo tofauti. Wayahudi kutoka kwa nchi mbali mbali waliwasikia wanafunzi wakizungumza kwa lugha zao. Wayahudi walishangaa.

Wayahudi hawakuelewe vile wanafunzi walizungumza hizi lugha zote. Waliuliza, “Hawa watu wanazungumza hizi lugha namna gani? Hawajajifunza hizo lugha. Tunatoka nchi nyingi za lugha mbali mbali lakini mbona tunawaelewa wakinena?”

Watu wachache waliwafanyia msaha. Walisema, “Hawa watu wamelewa.” Petro alisimama na akaambia huo umati, “Mnisikilize. Hawa watu hawajalewa. Ni saa tatu asubuhi! Haya ni maneno yenye nabii Yoeli aliyazungumzia. Mungu alisema kwamba atawapa watu wake Roho Mtakatifu. Nguvu za Roho Mtakatifu ndiyo zinawasaidia hawa watu kuzungumza hizi lugha nyingi.”

“Mliona miujiza zote zenye Yesu Kristo alifanya. Yesu ni Mwana wa Mungu. Lakini mlifanyia maovu na kumsulubisha. Mungu amemfufua Yesu kutoka kwa wafu. Sisi wote tumemwona Yesu baada ya kufufuka kutoka kwa wafu. Sasa Yesu ameenda kuishi na Mungu Mbinguni. Huyu Yesu mliyemsulubisha ni Mwana wa Mungu.”

Wayahudi waliposikia haya walifadhaika sana. Mungu alituma Mwanawe wapekee, ili awaokoe. Walikuwa wameuwa Mwana wa Mungu!

“Waliuliza Petro, “Tufanye nini?” Petro aliwambia, “Tubuni. Mbatizwe katika Jina la Yesu. Halafu Mungu atamsamehe.”

Wayahudi wengi walisikitika sana kwa sababu hao ndio walitaka Yesu asulubiwe. Walikumbuka vile walisimama nje ya Jumba la Hukumu ya Pilato. Walikuwa wamepasa sauti wakisema, “Msulibishe! Msulibishe!” Walikumbuka kwamba walifanyia Yesu msaha alipokuwa akifa msalabani. Waliabika sana. Waliomba Mungu awasamehe huo uovu. Halafu walibatizwa katika Jina la Yesu. Kama watu elfu tatu walibatizwa siku hiyo.

Huu ulikuwa mwanzo wa Ukristo. Watu wengi walibatizwa wakati wa Siku ya Pentekoste. Kukawa na kikundi kikubwa cha Wakristo Yerusalemu.

Wayahudi waliosafiri kutoka nchi mbali mbali, walirudi nyumbani baada ya Siku kuu. Wayahudi hawa walirudi kwao na Habari Njema. Walifundisha watu wa kwao kwamba Yesu ndiye Kristo na ni Mwana wa Mungu. Walianza vikundi vya Wakristo huko nyumbani kwao. Baadaye mitume kama Paulo walisafiri nchi nyingi wakihubiri Injili.

Mwishowe Injili ilikuja mpaka kwa nchi zetu pia.